

**KAZI YA LIKIZO**

**KIDATO CHA PILI**

1. Taja sifa tatu za kuzingatiwa katika utamkaji wa konsonanti. (Alama 3)

2. Taja viungo viwili vinavyozingatiwa katika utamkaji wa irabu (Al.2)

3. Eleza maana ya :

Konsonanti hafifu

Konsonanti ghuna (al 2)

4. Kwa kutumia ritifaa Onyesha mahali mkazo unawekwa kwa neno: (al.2)

Chwelea

5. Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo wingi. (al.2)

Mbwa wake ana meno makali.

6. Eleza matumizi ya “na” katika sentensi . (alama 3)

Musa na Ondari wanaandaliwa chakula na Kerubo.

7. Mofimu ni nini? (al. 2)

8. Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha matumizi ya kiimbo. (alama 2)

9. Taja ngeli za nomino zifuatazo :

a) Sandurusi

b) Saa

c) Asali

d) Mti

e) Nyumba

10. Tunga sentensi kudhihirisha maana za vitate vifuatavyo. (al. 2)

a) Bure

b) Pure

11. Kamilisha tanakali za sauti zifuatazo. (al. 2)

Maji yalijaa

Barabara imenyooka

12. Andika katika hali ya ukubwa wingi. (al. 2)

Msichana mrembo ameolewa na mwanamume hodari.

13. Eleza tofauti za sentensi hizi: (al.2)

Nilimpata huku.

Nilimpata humu.

14. Eleza mofimu zilizo katika neno hili. (alama 2)

Lililolila

15. Tunga sentensi ukitumia kinyume cha kitenzi hiki: (al.2)

Ezeka

16. Yakinisha sentensi ifuatayo: (al.2)

Tusingalienda hospitali,tusingalitibiwa.

(17) Unda nomino kutokana na utenzi. (alama 1)

Chelewa

ii) Andika

(18) Neno 'huyu' limetumikaje (kumaanisha nini katika sentensi hizi) (alama 2)

(i) Huyu amekuja kwangu

(ii) Mgeni huyu amekuja kwangu

(19)Tunga sentensi ukitumia kielezi cha

(i) namna/jinsi. (alama 1)

(ii) Idadi. (alama 1)

(20) Kanusha sentensui ifuatayo. (alama 1)

Mlevi alitembea kiholela halafu akaanguka chini pa!

(21) Andika katika usemi wa taarifa.

(Alama 3)

“Karibu Bakari, tafadhali kaa’, Juma akasema.

“ Asante, Je, habari za nyumbani?” Bakari aliuliza

(22)Taja vielezi vinavyopatikana katika sentensi hizi; kisha eleza ni vielezi vya aina gani.

i) Alilala jioni.

(alama 1)

ii) Mchezaji huyu ni hodari sana.

(alama 1)

(22) Andika udogo wa sentensi zifuatazo

i) Sahani zetu ni nzuri kuliko zao.

(alama 1)

ii) Njia hii inaelekea kule mlimani.

(alama 1)

(23) Akifisha sentensi ifuatayo.

(alama 2)

nilimkuta mkuu wa wilaya ya fahari akisoma kitabu kiiwacho utubora mkulima.

(24) Eleza maana ya misemo ifuatayo.

(alama 4)

i) Msumari wa moto juu ya kidonda

ii) Giza la ukata

(25) Sahihisha sentensi ifuatayo kwa njia tatu tofauti.

(alama 3)

Hapo ndimo alikofia

### ISIMU JAMII ALAMA 20

“Semeni Amen. Na ndugu atamsaliti mtoto na watoto wataondoka juu ya wazazi wao na kuwafisha. Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kusaburi hata mwisho, ndiye atakayeokoka”.

Maswali

a)Eleza muktadha wa mazungumzo haya.

( alama 2)

- b) Fafanua sifa ya lugha iliyotumika katika mazungumzo haya. ( alama 5 )
- c) Eleza sababu zinazofanya mazungumzo yanayotokea katika mazingira mbalimbali kuwa na sifa tofauti tofauti za kimatumizi ya lugha. ( alama 8)
- d) Eleza umuhimu wa isimu jamii (alama 5)

**FASIHI SIMULIZI ALAMA 20**

- 1a) Fasihi Simulizi ni nini? ( Alama2)
- b) Fafanua dhima ya fasihi simulizi. (alama 9)
- c) “Fasihi simulizi na fasihi andishi zina uhusiano wa karibu sana” . Eleza. (Alama 9)

[Ecolebooks.com](http://Ecolebooks.com)



[DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM](http://EcoleBooks.com)